**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Naanza hotuba yetu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia uzima na afya njema na hii leo tukaweza kukutana tena katika Chombo hiki kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako kwa busara zenu na kwa kuliongoza Baraza hili tukufu kwa uadilifu mkubwa. Ni imani yetu kwamba mutaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki ambacho ni muhimu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutuletea maendeleo makubwa nchini, pamoja na wasaidizi wake Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Othman Masoud Othman na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,**

Sina budi pia, kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi pamoja na Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisisishia kazi ya kuongoza kikao kuwa nyepesi na ya ufanisi. Kwa kweli, ni Wajumbe mahiri ambao wameweza kuyajadili kwa kina na ipasavyo makadirio hayo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinishiwa zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Yahya Rashid Yahya — Mwenyekiti
2. Mhe. Aza Januari Joseph — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ameir Abdalla Ameir — Mjumbe
4. Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed — Mjumbe
5. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir — Mjumbe
6. Mhe. Mwanajuma Kassim Makame — Mjumbe
7. Mhe. Hassan Hamad Omar — Mjumbe
8. Mhe. Issa Haji Ussi — Mjumbe
9. Mhe. Simai Mohammed Said — Mjumbe

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi na makatibu watatu (3) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| 2. | Ndg. Saad Othman Saad | Katibu |
| 3. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Ikiumbukwe kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka kwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii. Hivyo, katika kutekeleza jukumu hilo la Kanuni, Kamati yetu ilikaa na kujadili na hatimae ikapitisha Makadirio ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo.

## MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha robo tatu imeweza kukusanya asilimia 99 ya mapato waliyopangiwa kutoka vianzio vyake vya mapato vya ndani. Ni matumaini ya Kamati kwamba Wizara imejipanga zaidi ili katika robo iliyobakia ikusanye zaidi na waweze kuvuka malengo ya ukusanyaji waliyowekewa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa mtiririko wa jumla wa fedha za matumizi, Kamati haikuridhika na asilimia 48 ya upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya shughuli za kila siku za Wizara hii. Kamati inaiomba Serikali kuiingizia fedha Wizara hii kwa wakati na kwa mujibu wa walivyoomba na walivyoidhinishiwa.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonesha Wizara inaendelea na juhudi za matayarisho ya Sera ya Maendeleo ya Miji na Sera ya Maendeleo ya Makaazi. Kamati ilipodadisi juu ya maendeleo ya sera hizi ilijuilishwa kwamba tayari zipo katika hatua za kupelekwa katika vyombo vya kutoa maamuzi ikiwemo Baraza la Mapinduzi. Kamati inaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla iharakishe taratibu ya kumaliza utayarishaji wa Sera hizo kwani zitasaidia katika upatikanaji wa ufanisi wa Taasisi mbalimbali zilizomo ndani ya Programu hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Sambamba na maelezo ya hapo juu, Kamati inahimiza Wizara kufanya mapitio ya Sheria ya Mthamini Mkuu wa Serikali ili hatimae iweze kuandaa Mswada wa Sheria ya Ofisi ya Mthamini Mkuu kwa lengo la kupata Sheria bora

itakayoongoza katika kupunguza malalamiko ya wananchi juu ya uthamini unaofanyika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati bado haijaridhishwa na maendeleo na utekelezaji wa Mradi wa Mfumo wa Usimamizi wa Usajili wa Taarifa za Ardhi (LARIS). Kamati inatoa msisitizo kwa Mradi huu kulingana na malengo yake mazuri ya kuimarisha shughuli za usimamizi wa ardhi ikiwemo upimaji, mipango miji, usajili, utambuzi na uthamini.

Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba hadi hivi sasa Wizara bado iko katika hatua ya kukamilisha nyaraka za mradi huu. Hivyo, Kamati inaomba kipaumbele cha Wizara hii kilenge katika utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini upungufu wa makusanyo ya mapato yanayokusanywa na Kamati ya Kudhibiti Ujenzi (DCU) katika ukusanyaji wa fedha zinazotokana na Ada za vibali vya ujenzi. Kamati ilipohoji juu ya mapungufu haya Wizara

ilifafanua kwamba suala hili limesababishwa na mkanganyiko wa majukumu kati ya DCU na Halmashauri za Wilaya zetu pamoja na Mabaraza ya Manispaa ambazo zote zinahusika katika makusanyo hayo. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuweka chombo kimoja madhubuti kitakachosimamia Vibali vya Ujenzi ambacho kitakuwa na nguvu za kisheria za kukusanya mapato yanayotokana na vibali hivyo.

**Mheshimiwa Spika**,

Wakati Kamati inachambua bajeti ya Afisi kuu Pemba, ilishtushwa na makisio ya matumizi yaliyowekwa katika Afisi hiyo, kwani Kamati imebaini kushuka kutoka Shilingi **1,054,004,000** kwa mwaka wa fedha 2023/24 hadi shilingi **864,936,000** kwa mwaka ujao wa fedha. Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba kushuka huko kwa bajeti kunatokana na kuhamishwa kwa Wakala wa Majengo ambayo sasa imehamishiwa Wizara ya Ujenzi, Mawasilino na Usafirishaji.

## PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,**

Ingawa Wizara kupitia Taasisi zake inajitahidi kufanyakazi kwa bidii katika shughuli mbalimbali za usimamizi wa Ardhi lakini bado Taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Kamati imebaini changamoto ya kukosa majengo ya kufanyia kazi na kusababisha Taasisi hizo kukodi majengo kwa gharama kubwa na malipo ya OC yakichelewa wanashindwa kulipa kodi hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia imebaini changamoto ya upungufu wa vyombo vya usafiri, uhaba wa wataalamu katika fani mbalimbali za Ardhi, pamoja na kutopata fedha za kutosha kama ilivyokadiria katika bajeti yake. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuzitatua changamoto hizi ili Wizara hii iweze kutekeleza majukumu waliyopangiwa ikiwemo kukusanya mapato yake kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MAKAAZI

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa udhati kabisa Kamati inaipongeza Idara ya Maendeleo ya Makaazi kwa kuweza kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato kupitia Ada ya Usajili wa Kondominio hadi kufikia asilimia 206. Licha ya Idara hii kuvuka malengo ya Ukusanyaji Kamati inashangazwa na Uingizwaji wa Fedha katika Programu hii Kupitia Idara ya Maendeleo ya Makazi kwani katika kipindi cha Miezi tisa tumebaini kwamba imeiingiziwa asilimia 46 tu za makadirio. Kamati inaihimiza Serikali kuwaingizia fedha walizoidhinishiwa kwa wakati ili waendelee kuchapa kazi na kukamilisha malengo waliyopangiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kufikiria kuwa na bajeti ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu kama inavyooneka katika fungu kuu hili. Kamati inaiomba Wizara katika ujenzi wa nyumba hizo wawe makini katika utekelezaji wake na kuhakikisha wananchi wenye kipato cha chini ndio watakaofaidika na mradi huo, badala ya nyumba hizo kununuliwa na watu wenye uwezo mkubwa wa kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia Kamati imebaini kwamba majukumu mengi ya Taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kiasi kilichopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**

Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie na hatimae waipitishe Bajeti ya Wizara hii kama walivyoomba ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake kutimiza malengo waliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati yangu ***Naomba kuwasilisha na Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

…………………………………

**Yahya Rashid Abdulla**

Mwenyekiti,

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**